

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS

Anuani ya Simu: "TAMISEMI"
Simu Na: (026) 2322848, 2321607
2322853, 2322420
Nukushi: (026) 2322116, 2322146
2321013
Barua pepe: ps@tamisemi.go.tz



Tawala za MKOA na
Serikali za Mitaa,
Jengo la Mkapa,
2 Barabara ya hospitali,
S.L.P. 1923,
41185 DODOMA.

Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. Na. CD. 162/355/01/68

9/2/2018

TANGAZO LA KUITWA KAZINI

OR TAMISEMI inapenda kuwataarifu wale wote walioomba kazi kuanzia tarehe **25/07/2017** hadi tarehe **11/08/2017** kuwa mchakato wa kuwapangia vituo vya kazi kujaza nafasi za watumishi ambao walipangiwa vituo vya kazi na kushindwa kuripoti kazini.

Waombaji wote waliopangiwa vituo vya kazi wanatakiwa kuzingatia maelekezo yafuatayo:-

- i) Kuripoti katika vituo vya kazi walivyopangiwa katika muda wa siku kumi na nne (14) kuanzia tarehe ya tangazo hili. Aidha, waombaji watakaoshindwa kuripoti kwenye vituo vya kazi ndani ya siku kumi na nne (14) nafasi zao zitajazwa na waombaji wengine haraka iwezekanavyo.
- ii) Kuwasilisha kwa waajiri wao vyeti halisi (**Originals Certificates**) vya masomo kuanzia kidato cha nne na kuendelea kwa ajili ya kuhakikiwa na waajiri kabla ya kupewa barua za ajira.
- iii) Hakutakuwa na mabadiliko ya vituo vya kazi kwa kuwa lengo ni kujaza maeneo yaliyo wazi baada ya watumishi waliopangiwa hapo awali kushindwa kuripoti.

Orodha ya majina ya waombaji waliopangiwa vituo vya kazi inapatikana kupitia tovuti ya OR TAMISEMI www.tamisemi.go.tz.

Kwa waombaji wote ambao majina yao hayakuonekana katika tangazo hili, watambue kuwa hawakupata nafasi hivyo wasisite kuomba kwa mara nyingine nafasi za kazi zitakapotangazwa.

Limetolewa na:-



Rebecca Kwandu

Mkuu wa Kitengo cha Habari na Mawasiliano Serikalini

OR - TAMISEMI

9/2/2018